BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

DEODORANT SPRAY
YA MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

Kwa Nini Hawa Waislamu Wenzetu Wanatutesa Hivi?

INASIKITISHA kuona kila wa mwezi wa Ramadhani unapowadia, vyakula vinapanda bei "*haramu*" na kati ya wanaopandisha bei ya bidhaa muhimu bila shaka ni Waislamu wenzetu ambao kwa vyovyote wangelifikiria juu ya wenzao hasa wenye uwezo wa hali ya chini.

NILIWAHI kutembelea jijini Nairobi nyakati za karibu na sikukuu ya Krismasi, na nikavutiwa mno na Jinsi wenye biashara hasa za nguo pamoja na bidhaa nyingine walivyopunguza bei. Hii walifanya ili Wakristo wengi zaidi waweze kununua nguo hizo na kusherehekea vyema siku kubwa yao.

LAKINI ndugu zangu Waislamu ingawa ukweli ni uchungu, lazima tuanze kufikiria hali za Waislamu ambao wamekuwa wakiteseka kila Ramadhani inapowadia. Maduka yakiwemo ya wale wafanya biashara wa Kiislamu hupandisha bei pengine usiku wa kuamkia siku ya kwanza ya Ramadhani.

HII yote inaonyesha kwamba sisi wenyewe Waislamu hatuoneani imani. Kuna wengine wana pesa zao wanaweza kununua vitu vya ghali kwa mwezi mzima wa Ramadhani, lakini je, kwa wale wasio na uwezo? Lingekuwa jambo la busara kwa wafanya biashara wa Kiislamu kuzingatia mafunzo ya dini na kufikiria wasiojiweza.

KWA wakati huu vyakula kadha vimepandishwa bei bila idhini yoyote ya Serkali ama kwa wanaohusika kuweka bei za bidhaa. Kunde ambazo siku chache zilikuwa zikiuzwa kwa 7/- kwa kilo sasa hupati kama huna 16/- ama 20/- kwa kilo moja. Hali kadhalika njugu mawe zapatikana 20/- kwa kilo.

VIAZI vilikuwa vikiuzwa 4/- kwa kilo kabla ya Ramadhani kuingia. Sasa ukitaka viazi hupati kama huna 6/- kwa kilo. Ndizi za tamu hali kadhalika zimepanda na nazi ndio kabisa kwani bei mpya ya nazi imepita 100% kwa bei ya zamani. Ni vingi vilivyopandishwa na sisi tuna wajibu wa kuwalaumu wachuuzi walio Waislamu ambao ndio chanzo cha maongezo hayo.

HATUNA budi kulaani vikali wale Waislamu ambao wanajitakia faida kubwa kwa kuongeza bei za bidhaa zao hasa kwenye kipindi hichi kigumu ambacho wazazi wanakwenda mbio kutafuta riziki za futari na daku na pia nguo za watoto ambao wanazihitaji nyakati za kusherehekea Idd El fitr. Waislamu wanaoengeza bei za bidhaa zao nyakati hizi afadhali waweke maandishi ya "*MAONGEZO*" badala ya yale wanayoweka ya "*SALE*" waseme ukweli! - **ABDULRAHMAN SHERIFF**

Mabibi Waswali Mswalani

MSIKITI wa Mswalani umekamilisha gorofa mpya ya mabibi kuswalia swala ya Ijumaa na tarawehe. ameeleza Imam wa Msikiti huo. Ustadh Khamis aliyewashukuru wale wote waliojitolea kwa hali na mali kuona jengo limekamilika wakati wa mwezi huu wa Ramadhani.

Ustadh Khamis pia amewashukuru wanakamati wa misikiti miwili- Mswalani na Mlango wa Papa kwa kuafikiana Swala ya Ijumaa iwe ikiswaliwa Mswalani ili nao mabibi wapate fursa ya kuswali.

Hili ni jambo la tarekhe kubwa kwa akina mama wa mji wa kale kuswali jamaa na waume katika msikiti mmoja. Mabibi wanaoingia msikiti huo wana mlango wao maalum na pia mahali pao pa kutawadhia.

Waislamu Wajiepushe Na Kujikanya Machafu Yote

na. F. DUMILA

MWEZI MTUKUFU wa Ramadhani unawapatia waumini wa Kiislamu mafunzo chungu nzima kama mafunzo ya kiroho, kiwiliwili, kijamii na malimwengu.

Ni katika mwezi huu wa Ramadhani Kurani ilipoteremeshwa ikitilia mkazo juu ya kujifunza yaani kusoma. Jambo la mwanzo Mtume Mohammad (S.W.A.) aliloamrishwa alifanye ni kusoma. Aliambiwa: "Soma kwa jina la Mwenye-ezi-Mungu aliyeumba. Aliyemumba Mwana-Adamu kutokana na kijipande cha nyama. Soma na Mola wako umtukuze."

Ni kutokana na Aya hii ya Mwanzo kuteremshiwa Mtume Mohammad ndio Waislamu huzingatia kwa makini umuhimu wa Elimu. Ni wajibu wa kila Mwislamu Kujifunza elimu hata ikiwa mbali vipi kwani inampasa Mwislamu kuifuatia elimu hata kama ipo nchi ya China.

Visa vingi muhimu katika historia ya Uislamu vilitokea wakati wa Ramadhani. Waislamu walipigana vita vikuu vya Jihad vya Badru. Wakati huo wanajeshi wa Ki-Islamu walikuwa ni wachache lakini walitiwa moyo na Aya iliyowaambia kwamba ni vikundi vingapi vidogo vilivyoshinda vikundi vingi kwa idhini ya Mola.

IMANI

Iliwathibitikia kwamba chombo kikubwa cha kupigania katika Jihadi ni Imani thabiti. Mwanajeshi akiwa na imani thabiti ni upesi kwake kushinda na kuendeleza yale madhumuni anayoyapigania.

Ni katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani kwa Waislamu wanatakiwa kujizidishe ushujaa wao na kugeza subira zao katika mambo magumu yanayowakabili katika maisha yao. Ni kuvumila njaa mchana kutwa ni sehemu moja tu ya matunzo ya kujinyima.

KIWANGO

Kwani mausiyo makubwa anayoyapata Mwislamu ni kujikanya asifanye maovu yenye kumfiksha katika kiwango cha umyama mashetani mwake. Mwislamu anatakiwa afanye kila bidii asiweze heshima yake, hima yake kuongokewa na mamba fisi na awe ni mtu katika jamii ambaye ni mwenye kutegemewa kwa fikira zake njema na vitendo vyake vizuri kwa jamii nzima iliyo nchini kwake.

MWADHINI: Waislamu Mombasa watafungua leo Ijumaa saa 12 na dakika 23 za magharibi; Lamu: 12.22; Malindi: 12.23

Tamarind Yasifiwa

MWENYEKITI wa Hoteli za Tamarind amewasifu wafanyakazi wa hoteli ya Tamarind ya Mombasa kwa kazi yao nzuri yenye ushirikiano bora ambayo imewezesha huduma bora ya vyakula na vinywaji kuwa katika hali ya juu.

Mwenyekiti huyo, Bw. Chris Seex alisisitiza umuhimu wa nidhamu ya kazi ambao unaonyeshwa na wafanyakazi wa Mombasa hata ukawa unaigwa na wenziwao kutoka Nairobi Tamarind na Carnivore. "Mfano huu umekuwa Chombo muhimu katika kuleta ufanisi wa hoteli zetu hapa nchini", alisema. Bw. Seex.

Bw. Seexe alikuwa akizungumza wakati wa sherehe za kutoa zawadi kwa wafanya kazi waliotumikia hoteli hiyo kwa vipindi vya miaka mitano na kumi. Wafanyakazo waliotunukiwa ni na Charles Willy Mkonga (dreva, miaka 10), Joseph Okinda (mpishi miaka 5), mlawi mwakazi Danson Iddi (naibu mpishi, miaka 5), saya ali mushi (mpishi, miaka 5), james wale (mhudumu wa baa, miaka 5), Hamisi Mwamrazi (msafishaji, miaka 5), Norman John (naibu afisa mgavi, miaka 5).

MAWAIDHA YA DINI

SHEIKH Abdul Abdallah wa Msikiti wa Mwalani akitoa mawaidha ya dini ya Kiislamu wakati huu wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Aliwaomba Waislamu wasiache kwenda msikitini kuswali. "Tushikeni swala wakati wote. Tuendeleeni kuswali daima na wala tusiache baada ya Ramadhani", Akaongeza.

Halaiki ya Waislamu kote nchini hujazana Misikitini kusikiza mawaidha ya dini ya Kiislamu yanayotolewa na wanayuoni na viongozi wa dini.

PICHA: CAESAR MADONGASHA

Farucci

BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA 'BINT EL SUDAN -

GIFT PACK' KWA WASHINDI WA PILI NA WATATU KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

CROSSWORD No. 188

KWENDA KULIA: 1. Wakati wa mvua kubwa. 5. Sumbua, kera. 7. Chombo cha mawasiliano. 9. Umoja wa mataifa. 10. Sehe moja ya mnyama. 11. Mnyama mjanja. 13. Piga mafungu. 14. Isipokuwa. 16. Kataa. 19. Mnyama wa kufugwa. 20. Coastweek.

KWENDA CHINI: 1. Maji yenye harufu nzuri. 2. Mji katika Tanzania. 3. Ama. 4. Inuka. 6. Katika duka. 8. Choma, tia sindano. 10. Mra haibadiliki. 12. Nguvu hasa za mungu. 15. Siku tuliyonayo. 16. Ufupi wa kitambulisho. 17. Yake kwa wingi. 18. Kama 20 kwenda kulia.

Majibu ya shindano la Fumbo la Kujaza Maneno No. 187. *Kwenda Kulia:* 1. FARUCCI, 6. DO, 7. MISHAHARA, 8. IS, 10. TAO, 12. IE, 13. WA, 14. LA, 15. AMUENI, 19. ENEZA, 20. KUA, 21. KENYA. *KWENDA CHINI:* 1. FUMBO, 2. UDHI, 3. COASTWEEK, 4. IWAPO, 5. CHANGAMKA, 9. KEMEA, 11. AANZE, 12. JA, 16. UN, 17. IAN.

Washindi waombwa wafike afisini mwa Coastweek.

WASHINDI WA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 187.

1. Thomas Nyawa, Sanduku La Posta Mazeras 5. School, P.O. Mazeras Mombasa. 2. Ghusun K. Swaleh, Sanduku La Posta 87003, Mombasa. 3. Riziki Juma Sanduku La Posta 90581, Mombasa.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yetakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata vitalu na 'Bint El Sudan - Gift Pack'. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK limited Mombasa. Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Mhariri COASTWEEK, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tarehe **June 20 1984** saa nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.

JINA.....

SANDUKU LA POSTA.....

.....

USIDANGANYIKE

na ISIHAKA MTAMBUA

NA LAU utawafuatafuata na uwatamshe maneno ya kuifuata dini ya Kiislamu ni wenye kukupuuza kutokana na hayo maneno yako. Katika vikundi kama hivyo kunapatikana wengineo wasioamini kamwe kama kuna dini ya Mwenye-ezi-Mungu na siku ya mwisho.

Usidanganyike na watu kama hao walioritadi. Wanapatikana vile vile wasiokiamini Kitabu Kitukufu "Qur'aan" na kukihishimu. Hufikia hadi wakasema inawezekanaje Qur'aan kumuongoza mtu!

Wamesahau majambo yote ya ulimwenguni na yale ya kesho akhera. uwezo wa Mwenya-ezi-Mungu na kadhalika umeelezwa katika Qur'aan. Qur'aan imekuja kwetu kama mawaidha na pozo kwa wale walio na nyoyo zenye magonjwa ya ukafiri.

Inafahamika watu bora katika wale wanaoritadi ni wale unapowauliza ama kuwalingania majambo ya Mola wao. hukujibu hatuna ujuzi nayo ama hayawaingii akilini mwao. Watu kama hao ni katika wale walioritadi. lakini jawabu zao si za kifedhuli.

Tunao ndugu Waislamu hadi wakati huu hawajaamua kuifuata dini ya Mwenye-ezi-Mungu na unapowauliza hukujibu hawajakadiriwa. Kuna wale waliozama katika elmu ya Kilimwengu inayofanyisha mawazo yao kupanuka na kuwapoteza busara na mazingatio.

Unaweza kuwasikia wanaulizana iwapo ni kweli Mwenye-ezi-Mungu yuko hai. na unapowajibu yupo daima. wao husema hawaamini kwa vile hawajamuona. Lakini ajabu watu kama hao utawaona wanazwali kufunga n.k. Na wendapo utawauliza ni kwa nini hasi wanazitekeleza hizo ngozo hukujibu tunatekeleza lanje tukuwa "Nyunga (Wanje wakaonekana wamejitenga na vitendo vya dini inayolwatwa na baba zao).

Wako wanaozitekeleza ibada zao kuwafurahisha babazao mamazao ama wamelazimishwa wazitekeleze hizo ibada na jamaa zao. Wanapatikana wengine wanaoingia misikitini kwa siku wanazopendeleza wao ama kuwafuata marafiki zao kwa vile wanatembea nao.

UBORA

Wanapokwenda kuwali hujiona wako pweke wanaoneleza ubora kujiingiza misikitini kuwaridhisha hao marafiki zao.

Kuna na wengine wanaoleleza ibada zao kutokana na kuamriwa na "Mashwetani" wa vichwani (Kama inavyodaiwa) kinyume na kutekeleza ibada kwa wajibu kwa Mola wao.

Hivi ni baadhi ya vitendo vilivyooteka Ulimwengu wa Kiislamu na kuzamisha

/MWISHO/